



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI MASASI

(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Unapojibu tafadhali taja:

MTC/B.10/3/172

Tarehe: 25/01/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa zilizo rodheshwa katika tangazo hili kuomba nafasi zifuatazo:-

MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (Nafasi 03).

SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na Elimu ya kidato cha nne (Form IV) au sita (Form VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada /Cheti katika moja ya fani za Utawala ,Sheria,Elimu ya Jamii,Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU.

- I. Afisa masuhuli na mtendaji Mkuu wa Serikali za Kijiji.
- II. Kusimamia Ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Mtaa.
- III. Kuratibu na kusimamia Upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Mtaa.
- IV. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- V. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- VI. Kuandaa taarifa za utekelezaji na kazi katika eneo lake na mkakati wa kuondoanjaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- VII. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalamu katika Kijiji.
- VIII. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Mtaa.
- IX. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- X. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Kijiji.
- XI. Kusimamia utungaji na utekelezaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- XII. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

MSHAHARA.

Ngazi ya mshahara TGS B₁

1. DEREVA DARAJA LA II TGS B - (Nafasi 2)

SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na Cheti cha Awali cha Mafunzo ya Udereva na Cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka bila kusababisha ajali.

MAJUKUMU YA KAZI

- I. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- II. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- III. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- IV. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- V. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- VI. Kufanya usafi wa gari, na
- VII. Kufanya kazi nyingine kadri anavyoelekeza na Msimamizi wake.

MSHAHARA.

Ngazi ya mshahara TGS B₁

MAELEKEZO YA JUMLA KWA WAO MBAJI

- A. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kati ya miaka 18 na usiozidi 45.
- B. Maombi yaambatanishwe na taarifa ya maelezo binafsi (Curriculum Vitae) ya muombaji ikionesha wadhamini watatu na taarifa zao sahihi namba za simu za muombaji na wadhamini, cheti cha taaluma, cheti cha kidato cha nne, cheti cha kuzaliwa, na picha mbili passport size (ziandikwe majina kwa nyuma).
- C. Testimonial na provisional statemant of results, hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita havitapokelewa.
- D. Waombaji waliostaafu/kustaafishwa, kuacha, kufukuzwa au kukoma Utumishi wa Umma kwa namna yeyote ile hawarusiwi kuomba isipokuwa kwa kibali cha katibu Mkuu Utumishi.
- E. Muombaji atakaye wasilisha taarifa za kughushi au taarifa za Uongo kulingana na kiwango au sifa za kielimu na taaluma aliyonayo atachukuliwa hatua za kisheria

kwa mujibu wa taratibu.

- F. Baruaa zote ziandikwe kwa mkono kwa lugha ya kiswahili au kiingereza.
- G. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
- H. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe cheti cha ulinganifu (Equivalent Certificate) kutoka baraza la Mitihani la Tanzania.
- I. Kwa waombaji wenye vyeti vya ngazi ya NTA level 4, NTA Level 6 na shahada maombi yao hayatafanyiwa kazi. kinachopokelewa ni Technician Certificate" (NTA level 5 na elimu ya cheti) tu.
- J. Mwombaji aliyejiendeleza hadi kupata ngazi ya NTA Level 6 na kuendelea haruhusiwi kuomba nafasi hizi kwa kutumia cheti cha NTA Level 5 kwa sababu ukifanya udanganyifu huu tutakapo hakiki vyeti kwenye mamlaka husika na kubaini una sifa zaidi ya NTA Level 5 hutaajiriwa na unaweza kushitakiwa kwa udanganyifu.
- K. Watakoachaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili pia kupitia tovuti ya Halmashauri www.masasitc.go.tz pamoja na mbao za matangazo.
- L. Mwombaji awe na kitambulisho cha NIDA au namba ya usajili ya NIDA.
- M. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **03/02/2023** saa tisa na nusu (9:30 mchana).

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:
Mkurugenzi wa Mji,
S.L.P447,
MASASI.


ANDREA KALINGA
KAIMU MKURUGENZI WA MJI
MASASI

MKURUGENZI WA MJI MASASI
S. L. P 447
MASASI

Nakala:-

Katibu Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya ajira katika utumishi wa umma,
S.L.P 2320,
DODOMA.